



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ عَمَلُوا مِنْكُمْ وَعَكِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَطِعُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخَلَفَ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيَسْكُنَنَّ هُنَّمَ دِينُهُمُ الظَّلَمُ وَلَيَسْبِلُنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَقْوَهُمْ أَمَّا  
يَعْدُونَنِي لَا يَشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Jumatano, 19 Rajab 1445 H

31/01/2024 M

Na: HTS 1445 / 21

### Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

[وَلَنَبْلُونَكُمْ بِشَيْءٍ مِنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَفْسٍ مِنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّقَارَاتِ وَبَشَرِ الصَّابِرِينَ \* الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمْ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّ  
إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

“Hapana shaka tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu  
na matunda. Na wabashirie wanao subiri, Wale amba o ukiwasibu msiba husema: Hakika  
sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Al-Baqara 2:155-156]  
(Imetafsiriwa)

Baada ya kuridhika na Qadhaa ya Mwenyezi Mungu (swt), Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan  
inamuomboleza kwa masikitiko makubwa zaidi aliyesamehewa, Mwenyezi Mungu akipenda:

**Sheikh Abdul-Fattah Othman Muhiyidin**

Ambaye alifariki dunia kwa hatma hii isiyopukika mnamo siku ya Jumatano asubuhi, tarehe 19  
Rajab 1445 H, sawia na tarehe 31 Januari 2024 M, katika eneo la Wad al-Mahdi mashariki mwa  
Khartoum. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amjaalie rehema na msamaha wake mkubwa,  
na aijaalie pepo ya juu kuwa ndio makaazi yake na kimbilio lake.

Marehemu alikuwa kinara wa amali na shauku katika kubeba Dawah ili kuregesha tena maisha  
kamili ya Kiislamu kuitia kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume tangu miaka ya  
sabiini. Nyumba yake ilikuwa mashukio ya wabebaji dawah. Alikabiliwa na kukamatwa katika jela za  
madhalimu akiwa katika njia ya kubeba Dawah. Misimamo yake ilikuwa ya kuheshimika, na alibaki  
imara licha ya ugonjwa amba o ulimkoshesha uwezo katika siku zake za mwisho.

Rambirambi zetu za dhati kwetu sisi wabebaji Dawah kwa kufiwa kwake, na rambirambi zende kwa  
familia yake, watoto wake, jamaa na marafiki zake.

[إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّ إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Al-Baqara 2:156]

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)  
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir  
katika Wilayah Sudan**